

**Matumizi ya misimu ya vijiwani katika lugha ya Kiswahili :**

**Mifano katika Jiji la Dar es salaam**

**Abdallah Ibrahim**

**M.A Kiswahili**

**Chuo kikuu cha Dar es Salaam, Taasisi ys Kiswahili, 2013.**

Utafiti huu unahus matumizi ya misimu ya vijiwani katika lugha ya Kiswahili, katika mkoa wa Dar es Salaam. Ulichunguza na kueleza misimu mbalimbali ya vijiwani na maana zake, makundi na rika linalopendelea zaidi kutumia misimu na sababu zake na faida na hasara za matumizi ya misimu hiyo. Watafotowa 90 walihojiwa kwa kutumia sampuli nasibu tarbakishi na mbinu za hojaji, mahojiao na ushuhudiaji. Utafiti huu umebaini misimu mbalimbali ya vijiwani inayotumika katika lugha ya Kiswahili na maana zake, makundi na rika linalopendelea zaidi kutumia misimu hiyo na faida na hasara za matumizi ya misimu ya vijiwani katika lugha ya Kiswahili. Mwisho utafiti huu umependekeza kuwa utafiti mwingine wa aina hii ufanyike katika mikoa mingine mbali na Dar es Salaam kwani misimu inatumika sana katika lugha ya Kiswahili kwa nchi nzima, pia kuchunguza vyombo mbalimbali vya habari vinavyotumia misimu ya vijiwani katika utangazaji wao na athari zake katika lugha ya Kiswahili nchini Tanzania, kueleza asili ya misimu ya vijiwani inayotumika katika lugha ya Kiswahili na kuchunguza ni kwa nini watu wenye umri kati ya miaka 31-45 na kuendelea hawatumii misimu ya vijiwani zaidi katika lugha ya Kiswahili nchini Tanzania.